

TANGAZO

TANGAZO

TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA



TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA  
WANAWKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, ambapo jumla ya shilingi **1,413,099,754.00** zimetengwa katika robo ya kwanza ya Mwaka 2024/2025. Hvyo vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika ofisi za kata zilizopo katika maeneo yenu. **Maombi yote yataombwa kwa kupitia mfumo wa kidigitali wa WEZESHA unaopatikana katika tovuti:**

<https://mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz>

### SIFA ZA VIKUNDI VITAKAVYOTAKIWA KUOMBA MKOPO

1. Wanakikundi wawe ni raia wa Tanzania, wenye akili timamu na umri wa miaka kumi na nane na kuendelea isipokuwa kundi la vijana ambapo kundi hili litakuwa ni kuanzia miaka 18 hadi 45.
2. Kikundi cha Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi(usajili) na Halmashauri.

3. Kikundi kiwe kinajishughulisha na ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.
4. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha Watu Wenye Ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2), kwa kuzingatia Kanuni ya 6 (1) Mtu Mwenye Ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya Manejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana nae katika eneo lake, aidha sifa zingine zinafanana na sifa za vikundi vingine.
5. Kikundi kiwe na akaunti benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajii ya shughuli za kikundi.
6. kikundi hakitajumuisha wajumbe wenye ajira rasmi.
7. Kikundi kiwe kimepata mafunzo ndani ya wiki sita mfululizo ambapo mafunzo hayo yatatolewa kwa siku moja kila wiki kwa mada tofauti tofauti na yatatolewa na maafisa waliopo katika maeneo yao.

#### **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

- i. Kikundi kitapoteza sifa za kukopa mkopo kama kitapoteza moja ya kanuni zilizoainishwa katika sifa za kupata mkopo hapo juu.
- ii. Hakijamaliza kurejesha mkopo uliotolewa chini ya kanuni hizi.
- iii. Kimetoa taarifa za uongo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa
- iv. Kimetumia fedha za mkopo kwa matumizi tofauti na yale yaliyoombewa mkopo bila idhini ya Timu ya Menejimenti
- v. Maombi ya nje ya mfumo hayatapokelewa.

- vi. Kikundi ambacho hakitahudhuria mafunzo hakitakuwa na sifa ya kupata mkopo.
- vii. Maombi yote ambayo yaliombwa awali kabla ya sitisho la mikopo Aprili 2023 **YAMEFUTWA**, hivyo waombaji wote wanatakiwa kufanya maombi hayo upya.

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA 03/11/ 2024**



HEMEDI S. MAGARO

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
KILWA